



BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Ishirini na Sita – Tarehe 02 Juni, 2022

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. MASWALI:

Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

83. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) -
Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na
Mipango:

Kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inaendelea kupokea
fedha zinazotokana na tozo za miamala ya simu.

- (a) Je, ni kiasi gani cha fedha kinapokelewa kila mwezi.
- (b) Je, ni miradi ipi imetekelezwa kupitia fedha hizo kwa Zanzibar.
- (c) Je, ni kwa nini fedha hizo matumizi yake yasiainishiwe maeneo maalumu.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

158. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Je, ni ajira ngapi za ukalimani wa lugha adhimu ya kiswahili ambazo wataalamu wetu wa lugha ya kiswahili Zanzibar wamefaidika nazo na ni nchi gani zinaoongoza kupata fursa hizo duniani.

Wizara wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

97. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kwa kuwa kilimo cha mazao ya viungo kama vile hiliki, abdalasini, uzile na kadhalika vina soko kubwa duniani, na kwa kuwa aina ya viungo hivi huwa ni tunu kwa Watalii.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha mazao hayo ili kulifikia soko la nje ya nchi.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

141. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Ni jambo jema kwamba Serikali imekusudia kuziboresha au/na kuzijenga upya barabara za ndani zilizo muhimu kiuchumi ndani ya visiwa vya Unguja na Pemba. Hata hivyo, mpango huo unaonekana kuchelewa na usio na uwazi.

- (a) Je, ni lini barabara ya ndani ifanyayo mzunguko (ring road) kutoka Mlindo kupitia Kiungoni na JKU Msaani na kumalizikia Mchangani itaanza kutengenezwa na lini itakamilika.
- (b) Je, ni ipi tathmini ya gharama za ujenzi wa barabara hiyo.
- (c) Je, ni katika hatua gani wananchi wataanza kushirikishwa katika ujenzi huo.

143. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani)

- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwa kuwajali wananchi wake, Serikali imekuwa ikifanya jitihada za kuviunganisha vijiji vidogo vidogo na sehemu zenye shughuli za kila siku za maendeleo. Hata hivyo, barabara na daraja inayoviunganisha vijiji vya Kivuugo na Wingwi hupitika baadhi ya misimu tu ya mwaka na takriban miezi mitatu kila mwaka hujaa maji na kutopitika kiasi kwamba wanafunzi hushindwa kwenda skuli na kukosa masomo yao wakati wenzao wakiendelea na masomo.

- (a) Je, Serikali inafahamu umuhimu wa barabara ya ndani inayounganisha vijiji vya Kivuugo na Wingwi.
- (b) Je, ni lini Serikali itaitengeneza barabara hiyo pamoja na daraja lake ambavyo hukatisha, kwa kiasi kikubwa, shughuli za wananchi misimu ya mvua.
- (c) Kwa vile matengenezo ya barabara hiyo kwa kiwango cha fusi yamewahi kutolewa ahadi na viongozi wetu wakuu, Je, kwa nini ahadi hiyo haijatekelezwa.
- (c) Je, Serikali haioni haja ya kuwaruhusu kufanya vipimo vya Uviko-19 (Covid Test) bila malipo kwa Wazanzibari wanaohitaji kufanya hivyo na ambao walikubali kuchanja kwa hiari.

II. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka 2022/2023.

Zanzibar,
02 Juni, 2022.


(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA